

IBADA

Je, ni Lazima Kupiga Magoti Wakati wa Maombi?

Kumekuwa na mijadala mingi hivi karibuni kuhusu upi ni mkao sahihi wakati mtu anapokuwa katika ibada ya maombi; hoja hizi zinatafuta kujua endapo daima tunapaswa kusali au...

MCH. ALMODAD AMOS YARAGWILLER

2026

Utangulizi

Kumekuwa na mijadala mingi hivi karibuni kuhusu upi ni mkao sahihi wakati mtu anapokuwa katika ibada ya maombi; hoja hizi zinatafuta kujua endapo daima tunapaswa kusali au kuomba tukiwa katika hali ya kupiga magoti pekee, au kama tunaweza kukaa au kusimama na bado Mungu akasikia sala zetu. Swali hili mara nyingi huibuliwa na baadhi ya ndugu wa imani ambao kwa minajili ya kujifunza kwao binafsi, wamehitimisha kuwa maombi yote yanayofanyikia kanisani yanapaswa kufanyika mtu akiwa amepiga magoti. Mjadala huu unaonyesha kwamba, maombi ni muhimu sana na yana maana kubwa katika ibada za jamii ya hao waaminio pamoja na mtu mmoja-mmoja. Watu wanataka kuhakikisha kwamba katika utendaji wao wanafuata maagizo ya Mungu kikamilifu bila kukosea.

Ingawa baadhi ya watu ndani ya jumuiya ya kanisa wanaamini kwa dhati kuwa kupiga magoti ndio mkao wa lazima kwa maombi, hasa wakati wa ibada ya pamoja, ni muhimu kuelewa kwamba usikivu wa Mungu kwa maombi yetu unavuka mipaka ya hali ya mkao wa kimwili tuliyo nayo. Hata hivyo ni muhimu pia kutambua kuwa shauku ya kushikilia kwa ukamilifu kile kinachoonekana kama “njia sahihi" ya kufanya maombi inaonyesha heshima kubwa ambayo wengi wanayo kwa kipengele hiki muhimu cha uhusiano wao na Mungu. Majadiliano haya hayalengi kupunguza umakini huu bali kutoa uelewa mpana zaidi wa mkao unaohitajika wakati wa maombi kulingana na Maandiko Yenye uvuvio ambayo hutupatia maelekezo kutoka kwa Mungu.

Kuomba kwa Kupiga Magoti

Mifano mingi katika Biblia inaonyesha watu wakipiga magoti katika maombi, ikionyesha kuwa ilikuwa desturi muhimu na ya mara kwa mara. Tabia thabiti ya Danieli ya kusali kwa magoti mara tatu kwa siku (Danieli 6:10), dua ya Stefano akiwa amepiga magoti kabla ya kuuawa kwake (Matendo 7:60), na tendo la Petro la kupiga magoti kabla ya kumfufua Tabitha kutoka kwa wafu (Matendo 9:40; rejea pia Matendo 20:36; Waefeso 3:14). Wakati mwingine, watu walikuwa wakiinamisha vichwa vyao hata vikutane na magoti yao wakati wa kusali (1 Wafalme 1:13). Kupiga magoti kunakoongelewa katika 1 Waf. 1:13 kwa kiebrania ni kujulikana kwa kitenzi *“kara”* [כָּרַע (*kā·rǎʿ*)**]** – tendo la kusujudu kwa kuinama kifudifudi mpaka chini, kichwa kikigusa chini au kikigusa magoti. Mara nyingi tendo hili liliashiria uhiari wa kujisalimisha kwa Mungu, ishara ya unyenyekevu ya kuanguka na kurudi mavumbini ambayo mwanadamu aliumbwa nayo.

Kuomba kwa Kusimama

Desturi ya kusimama mbele za Bwana wakati wa maombi ilikuwa desturi iliyokuwa imezoeleka zaidi na kuendea sana, hata zaidi ya desturi ya upigaji wa magoti. Mfano mzuri kabisa wa desturi hii njema unapatikana katika 2 Nyakati 20, wakati ambapo watu wa Yuda walikuwa wakikabiliwa kwa vita na Wamoabu, Waamoni na Wameuni; Biblia inasema walisimama mbele za Bwana huku Mfalme Yehoshafati, mwana wa Asa na mflame wa nne wa Yuda baada ya Israeli kugawanyika, akiwaongoza katika maombi yaliyomwekea Mungu ili awakomboe (2 Nyakati 20:5, 13). Biblia inatueleza pia kuwa Hana aliwasilisha ombi lake kwa Bwana akiwa

amesimama, na sala yake ilijibiwa (1 Samweli 1:26). Ayubu pia alishiriki katika maombi akiwa amesimama (Ayubu 30:20).

Ingawaje Yesu alikosoa unafiki wa wale waliosali wakiwa wamesimama hadharani ili waonekane (Mathayo 6:5), hakukemea hali ya kuomba mtu akiwa amesimama, isipokuwa alikemea unafiki wa kujionyesha. Ukweli kabisa ni kwamba Yesu hakupinga maombi yaliyofanyika mtu akiwa amesimama na alilithibitisha jambo hili alipowaagiza wanafunzi wake, "'Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. (Mk 11:25). Kusimama katika maombi kunaweza kuwa kumebeba maana yenye msisitizo wa fursa ambayo wanadamu wanayo ya kumkaribia Mungu kwa mahitaji yao, na kujua kwamba Mungu ni rafiki tunayeweza kumkaribia na kufanya mzungumzo naye kama rafiki pia. Mkao huu unafanana na jinsi mtu anayoweza kusimama mbele ya mfalme kuwasilisha ombi, ni ishara ya kumkiri Mungu kama mfalme wa ulimwengu na kuthamini fursa ya kutafuta uongozi Wake na baraka.

Kuketi

Ingawa si kawaida sana, Biblia inaandika matukio ya kusali huku mtu akiwa ameketi. Mfalme Daudi, kwa mfano, "... akaingia, akaketi mbele za BWANA, akasema..." (2 Samweli 7:18). Mkao huu mara nyingi ulionyesha utayari wa kutafuta na kupokea maagizo kutoka kwa Bwana, mara nyingi kupitia nabii (mfano, 2 Wafalme 4:38; Ezekieli 8:1; 33:31), na kuwa tayari kutumika.

Kulala

Sala pia zilitolewa pia watu wakiwa vitandani, hasa wakati wa usiku. Katika nyakati hizi, watu walimkumbuka Bwana na kutafakari juu Yake (Zaburi 4:4; 63:6). Wakati mwingine, mtu angeinama au kujinyoosha kitandani ili kusali (1 Wafalme 1:47). Kusali ukiwa umelala chini kunasisitiza kipengele cha hali ya kutafakari na kuingia katika maombi, na fursa ya kutafakari juu ya wema wa Mungu na kutafuta msaada Wake katika utulivu wa usiku. Ikiwa utatafakari jambo hili katika nuru ya mafunuo ya Nabii Ellen G. White, “maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki,” na hii inatukumbusha na kuweka msisitizo mkubwa kwamba maombi yanashughulika zaidi na uelekevu wa moyo kwa Mungu, kabla ya kushughulika na mkao wa kimwili. Jambo hili ndilo huongoza mengine yote yanayoweza kufanyika wakati maombi yanapofanyika.

Kulala Kifudifudi

Mkao huu ulihusisha kulala kifudifudi huku uso ukiwa chini, mara nyingi mikono ikiwa imenyoshwa. Ingawa mara kwa mara ulihusishwa na maombi (1 Wafalme 1:47; Marko 14:35), kimsingi ulikuwa ni onyesho la heshima kubwa ya kujinyenyekeza kwa viwango vya juu sana kuliko inavyoweza kuelezeka. Kuangaka huku katika lugha ya Kiyunani kunajulikana kwa neno “pipto” ambacho ni kitenzi [πίπτω (*piptō*)] – maana yake ni kulala chini na kujinyoosha kabisa. Utamaduni huu mara nyingi ulionekana wakati watu walipotafuta kwa hali na mali kibali cha mfalme; wangejinyoosha kwa kwa kulala chini kama ishara ya unyenyekevu na uwasilishaji wa mahitaji ambayo kwa kweli yalikuwa mahitaji makuu sana na makubwa mno (2 Samweli 14:4), wakati

mwingine jambo hili lilifanyika kama tendo la salamu kwa watu wenye nafasi za juu sana ambao hata wangetoa amri ya uhai wa mtu kuondolewa kwa amri moja tu (2 Samweli 14:22) au kuonyesha heshima (1 Samweli 28:14). Katika muktadha wa kidini, kujinyoosha kuliwakilisha tendo la ibada (tazama 2 Nyakati 20:18), kwa kukazia imani kwamba Mungu ndiye chanzo na mtunzaji wa uhai (Mfano, Yoshua 7:6; 2). Hii nayo ilikuwa ni moja miongoni mwa mikao ambayo waliofanya ibada walikaa wakati wakifanya ibada ya maombi.

Hitimisho

Uchunguzi makini wa Maandiko Mtakatifu unaonyesha kwamba hapakuwa na mkao mmoja uliolazimishwa kwa nyakati zote kwa waabudu walipokuwa wakimwomba Bwana. Badala yake, mikao mbalimbali ilitumika kama onyesho la nje la heshima, hisia za ndani, na kujitoa kikamilifu kwa Bwana. Hakika mikao hii mbalimbali ilionyesha pande mbalimbali za uzoefu wa aina mbalimbali, na hakuna moja ya mkao wa sala uliokataliwa na Mungu

Ellen G. White mara nyingi alihimiza kufanya maombi kwa magoti, akisisitiza kuwa hiyo ni fursa. Aliandika akisema, "Katika ibada ya hadhara na ya faragha, ni fursa yetu kuinama kwa kupiga magoti mbele za Bwana tunapotoa maombi yetu Kwake" (*Gospel Workers*, uk. 178). Aliongeza kwamba, "katika ibada ya hadhara na ya faragha ni wajibu wetu kusujudi kwa magoti yetu mbele za Mungu tunapotoa maombi yetu Kwake. Tendo hili linaonyesha utegemezi wetu kwa Mungu" (*Special Testimonies*, vol. 2, uk. 312).

Hata hivyo, kauli hizi hazipaswi kutumiwa kufundisha kuwa mkao pekee unaofaa kwa maombi katika ibada ya hadhara ni kupiga magoti. Ellen G.

White mwenyewe alifafanua kwamba si lazima kupiga magoti kila wakati tunapokuwa katika maombi (*Ministry of Healing*, uk. 510-511). Ushiriki wake mwenyewe katika ibada za hadhara wakati mwingine ulijumuisha nyakati ambazo aliuomba mkutano kusimama kwa ajili ya sala ya kujiweka wakfu (*Special Testimonies*, vol. 3, uk. 268, 269), wakati mwingine aliwaomba kubaki wakiwa wameketi wakati wa sala (ibid., uk. 267-268), au kupiga magoti (*Special Testimonies*, vol. 1, uk. 148-149). Hii inaonyesha kwamba Ellen G. White hakuchukulia kupiga magoti kama mkao pekee wa maombi kanisani. Zaidi ya hayo, utamaduni wake yeye binafsi ulihusisha kuomba akiwa ameketi kitandani (*Review & Herald*, Desemba 13, 1906).

Ili kuhitimisha na kumaliza tafakari hii, tunaweza kusema kuwa kulingana na Biblia na maandiko ya Ellen G. White, kuna mikao mbalimbali tunayoweza kuwa nayo na kuifanya kwa kicho wakati tunapokuwa katika maombi, na umuhimu wa mkao mmoja haupunguzi uhalali wa mkao mwingine. Mungu anasikia sala za watu waombao kwa kufungua moyo watafanya zala zao wakiwa katika hali ya kuketi, kusimama, au kupiga magoti. Kwa kuwa ibada inapaswa kuwa na utaratibu, ni muhimu kwamba wakati jumuiya ya waumini inapokusanyika kumtafuta Bwana, jumuiya hiyo ifuate kawaida za ibada ya utaratibu uliowekwa na kukubaliwa na waabudu husika.

Kwa hiyo basi, tunaweza kusema kwa ujasiri wenye msimamo wa uelewa wa maandiko kwamba: kuchagua mkao mmoja wakati wa maombi na kuuchukulia kwamba mkao huo ndio bora zaidi na wa lazima kuliko mwingine hakuna msingi katika maandiko yenye uvuvio.

Zaidi kutoka Injili Milele

Makala, vitabu, video na sauti zaidi zinapatikana kwenye maktaba ya Injili Milele:

Je, Sabato Ilikoma kwa Kuwa Ilikuwa Kivuli cha Mambo Yajayo?
Sabato · PDF

Sanduku la Agano: Je, Litaonekana Tena?
Unabii · PDF

Nini Hasa Maana ya Kibiblia ya Maneno ya Baba: “Mimi Leo Nimekuzaa”?
Uungu · Video

Je, Yesu ni “Mungu Mwana” au “Mwana wa Mungu”?
Uungu · Video

Kwa Nini Mungu Alimuumba Lusifa?
Pambano Kuu · PDF

Papa Gregory XIII Alipobadilisha Kalenda: Siku Zilivurugwa, Sabato Ilipotea?
Sabato · PDF

Injili Milele

almodad-2.github.io/injili-milele/sw/

WhatsApp +255 718 834 621 · modaofhope@gmail.com

© 2026 Pr. Almodad Amos Yaragwiller · Injili Milele. Haki zote zimehifadhiwa. Usiuze nakala hii bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi.